**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**
**MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI**
**VETA IRINGA**

---

**BARUA YA KUJIUNGA NA CHUO NGAZI YA KWANZA IRINGA RVTSC 2025**

Ndugu,

.......................................................................................................

Yah: **KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI STADI NA HUDUMA IRINGA (RVTSC) MWAKA 2025**

**MAELEZO HAYA YASOMWE KWA MAKINI NA MZAZI/MLEZI NA MWANAFUNZI**

1. Unafahamishwa kwamba umechaguliwa kujiunga na chuo tajwa hapo juu katika

   fani ya : .......................................................................................
   Ngazi ya Kwanza (Level One) Kutwa ☐ /Bweni ☐

2. Mafunzo yatachukua muda wa miaka mitatu kwa fani ya Upishi na Huduma ya chakula na vinywaji, miaka miwili na nusu kwa fani ya Uhazili na miaka miwili kwa fani zingine.

3. Chuo kitafunguliwa Rasmi Tarehe **13 Januari 2025**
4. Unatakiwa kuthibitishwa na Daktari wa Hospitali ya Serikali kuwa una afya nzuri ya kumudu mafunzo katika fani uliyopangiwa kwa kujaza fomu maalum (Medical Examination Form) iliyoambatanishwa.
5. Kwa kila mwanachuo aliye na umri wa miaka 18 au zaidi anapaswa kuwa na **namba ya NIDA** na kuiwasilisha chuoni siku ya kuripoti. Ikiwa unacho kitambulisho cha Bima ya afya ulichopewa na Mzazi/Mlezi hupaswi kulipa fedha ya Bima ya Afya bali uje na kitambulisho chako ambacho hakijaisha muda wa Matumizi.
6. Unatakiwa kuthibitisha wewe mwenyewe na Mzazi/Mlezi/Mdhamini wako kwamba unakubali nafasi ya mafunzo uliyopangiwa kwa kujaza fomu maalum iliyoambatanishwa kwenye barua hii.
7. Unatakiwa kufuata sheria na taratibu zote za chuo zilizoambatanishwa kwenye barua hii mara utakapofika chuoni.
8. Unatakiwa kufika chuoni na barua hii siku ya kuanza mafunzo

9. Unatakiwa kununua vifaa vilivyotajwa hapo chini katika barua hii kwa matumizi yako binafsi uwapo chuoni.
10. Unatakiwa kuleta kivuli cha cheti cha kumaliza shule na cheti cha kuzaliwa.
11. **Nafasi yako itapotea** kama utashindwa **kuripoti wiki mbili baada ya tarehe ya kufungua chuo.**

**MAHITAJI YA MWANAFUNZI ATAKAPORIPOTI CHUONI**

*Unatakiwa uwe na vifaa vifuatavyo:*

1. Mashati mawili (2) meupe mikono mifupi ya "Tetron" ***Kwa wavulana tu*** *na kwa* ***wasichana*** *blauzi (2) nyeupe (nusu kanzu)*
2. *Unatakiwa kuja na suluari (2) za rangi ya dark blue (sample ya kitambaa inapatikana chuoni.*
3. *Unatakiwa uje na overall kwa fani zote isipokuwa fani ya uhazili, mapishi na Huduma za hotel.*
4. *Kwa fani ya uhazili uje na overcoat rangi nyeupe.*
5. *Kwa fani ya mapishi na Huduma hotelini uje na apron nyeupe,kofia nyeupe zenye malighafi ya pamba (isiwe tetron) kwa ajili ya kuvaa wakati wa mafunzo kwa vitendo.*
6. *Uje na truck suit (**Dark blue nyenye mistari myeupe**) kwa wavulana na rangi ya **maroon (damu ya mzee) nyenye mistari myeupe kwa wasichana**.*
7. Jozi mbili za viatu vyeusi vya Ngozi vyenye visigino vifupi
8. Daftari 8 kubwa za kuanzia quire 2 na kuendelea kwa fani zote isipokuwa kwa fani ya Uhazili ambayo inatakiwa uje na daftari 12.
9. Vifaa vya somo la Hesabu (Mathematical set)
10. Karatasi nyeupe (A4) ream moja aina ya Mondi MAESTRO, SINARLINE, au TRION
11. Sweta 2 rangi ya Blue
12. Kwanja moja kwa Wasichana wote,Wavulana walete Jembe moja kwa fani ya Umeme na Magari, Reki moja kwa fani zingine zote.
13. Soksi rangi nyeupe kwa Wasichana na rangi nyeusi kwa Wavulana.
14. Viatu vya karakana aina ya "Safety boots" kwa ajili ya usalama utakapokuwa Karakana isipokuwa fani ya Uhazili (SCA), Mapishi na Huduma za Hoteli.
15. **Kwa mwanafunzi wa bweni** awe na godoro la futi (3 X 6), mto wa kulalia, blanketi, shuka 2 na foronya zake **za rangi ya blue kwa Wavulana na za rangi ya Pink kwa Wasichana**, chandarua, ndoo, sahani, kikombe, kijiko, nguo za kujikinga na baridi utakapokuwa bwenini, pamoja na vifaa vya usafi binafsi.

**MCHANGANUO WA MALIPO**

| NA | MAHITAJI | KWA MWANAFUNZI AMBAYE NI MTANZANIA | | | | KWA MWANAFUNZI AMBAYE SI MTANZANIA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | MWANAFUNZI WA KUTWA | | MWANAFUNZI WA BWENI | | KUTWA | BWENI |
| | | MUHULA I | MUHULA II | MUHULA I | MUHULA II | | |
| 1. | Ada ya Mafunzo | 30,000 | 30,000 | 60,000 | 60,000 | 360,000 | 680000 |
| 2. | Ada ya Mtihani | 25,000 | | | | | |
| 3. | Bima ya afya | 50,400 | | 50,400 | | | |
| 4. | Fulana/T-shirt | 15,000 | | 15,000 | | 15,000 | |
| 5. | Kitambulisho | 5,000 | | 5,000 | | 5,000 | |
| 6. | Nembo za VETA | 5,000 | 2e | 5,000 | | 5,000 | |
| 7. | Michezo | 15,000 | | 15,000 | | 15,000 | |
| 8. | Uchakavu na Mazingira | 20,000 | | 20,000 | | 40,000 | |
| 9. | Picha (passport size) | 3,000 | | 3,000 | | 3,000 | |
| **JUMLA** | | **168,400/=** | **30,000/=** | **173,400/=** | **60,000/=** | **443,000/=** | **680,000/=** |

**ZINGATIA:**

I. Kwa Mwanafunzi ambaye si Mtanzania lazima uje na Kibali cha kuishi Nchini, Hati ya kusafiria (Passport) ambayo haijaisha muda wake na utajaza fomu ya utayali wa kufuata Sheria kanunui na taratibu za Nchi yetu pendwa ya Tanzania.

II. Baada ya kulipa fedha benki wanachuo wote waje na risiti ya benki iliyoandikwa jina la mwanachuo kisha kuiwasilisha ofisi ya uhasibu ili wabadilishiwe na kupewa risiti ya VETA.

III. Bima ya afya ni lazima kuwa nayo kwa kila Mwanafunzi.Isipokuwa kama unayo kadi ya bima ya afya uliyopewa kupitia mzazi/mlezi hupaswi kulipa fedha ya bima, unatakiwa uje na kadi yako kwa ajili ya uhakiki.

IV. Ada ya mtihani Tsh. 25,000/= italipwa peke yake kwa “control number” inayopatikana Ofisi ya Msajili na italipwa mara tuu ufikapo kuripoti chuoni.

Kabla ya kulipa ada na michango mingine, fika chuoni upewe utaratibu wa namna ya kulipia. Ikiwa ni pamoja na namba ya malipo ya Serikali (Control Number) ya kulipia ada, Bima ya Afya, Mtihani na michango mbalimbali. **Hatupokei fedha taslimu.**

***V.*** Unatakiwa kulipa kiasi cha fedha kama kilivyo ambatanishwa kwenye barua hii. Hutapokelelewa chuoni iwapo utafika bila kutekeleza vifungu vilivyotajwa hapo juu. Lipa fedha kiasi ulichoagizwa tu. ***Fedha ikishalipwa hairudishwi***

**MAELEZO MENGINE UTAELEKEZWA UFIKAPO CHUONI AU PIGA SIMU NAMBA 0757 450 670**

Pasiens Nazary Nyoni
Mkuu wa Chuo
<u>VETA IRINGA</u>

MKUU WA CHUO
CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI STADI
NA HUDUMA
S.L. P 778 IRINGA

**VIAMBATANISHO**

I. Medical Examinations form
II. Sheria za Chuo
III. Fomu ya kukubali nafasi ya Mafunzo ya Ufundi